(Swahili) kiswahili

Kutuhusu

Karibu!

Department of Parks, Recreation and Waterfront (Idara ya Mbuga, Bustani na Kingo za Maji) inasimamia zaidi ya Mbuga 35, zaidi ya Ekari 550 za Ardhi ya Umma, Fukwe 4 za Umma, Miti kwenye Kingo za Barabara na Njia Zinazozingirwa na Miti, Bustani za Umma, Makaburi 3, Miller Recreation Center, Leddy Ice Arena, Champlain Senior Center, North Beach Campground, Community Boathouse Marina na Mipango yote ya Burudani mjini Burlington.

Azma Yetu

Kuunganisha maeneo na mipango mbalimbali ya umma inayokuza, inayohamasisha na inayowezesha utangamano wa kijamii kupitia ardhi, maji na watu.

Lengo Letu la Kudumisha Utofauti na Usawa

Mazingira (ya kazini) yanayozingatia na kudumisha usawa kupitia kufanya maamuzi jumuishi na kuchukua hatua zinazofaa kila siku.

Maadili ya Idara Yetu

Upatikanaji – Inasisitiza kanuni kuu zinazohusu utaratibu na uzingatiaji wa masuala ya kifedha kila wakati.

Uadilifu – Kuaminika tunapotekeleza majukumu yetu kwa umma.

Kutegemeka – Kutoa huduma na kuwashughulikia wateja.

Afya na Siha – Kufanya mazoezi, kuzingatia afya na kuishi inavyostahili.

Umoja/Ushirikiano – Kufanya kazi pamoja na kushirikiana na wafanyakazi-wenza na jamii yetu.

Ujumuishaji – Kuzingatia utamaduni wa watu wote.

Uwajibikaji – Kuhudumia umma na kudumisha mazingira endelevu.

Ubora – Katika utendakazi wetu wote.

Sera ya Mji Inayopiga Marufuku Ubaguzi: The City of Burlington (Mji wa Burlington) umepiga marufuku unyanyasaji au ubaguzi usio halali kwa misingi ya kisiasa, kidini, rangi, kabila, asili, mahali pa kuzaliwa, ukoo, umri, jinsia, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, hali ya ndoa, ukongwe, ulemavu, kuugua UKIMWI, uhasiriwa wa uhalifu au maelezo ya kijeni. The City (Mji) pia imejitolea kutoa huduma, vifaa vinavyohitajika, na fursa za ajira. Ili upate maelezo kuhusu ufikivu au miundo mbadala, tafadhali wasiliana na Idara ya Rasilimali Watu kupitia nambari (802) 540-2505.

Rules and Regulations (Sheria na Masharti) ya Bustani

Huenda sheria na masharti yakawa tofauti katika maeneo mbalimbali, kwa hivyo tafadhali angalia kanuni zilizochapishwa mahali ulipo. Baadhi ya sheria za kawaida zimeorodheshwa hapa chini. **Ili upate maelezo zaidi, tafadhali bofya hapa ili uangalie City Ordinances of Burlington (Sera za Mji wa Burlington).**

Kanuni kwenye Njia Zilizozingirwa na Miti

- **Nenda taratibu.** Endesha polepole mahali palipo na watu wengi. Tunajua kuwa wakati mwingine huwa kuna msongamano wa watu kwenye sehemu fulani za Njia.
- **Waendeshaji baiskeli sharti wawapishe wanaotembea.** Wanaotembea kwa miguu wanapaswa kupewa nafasi kila wakati. Wanaoendesha baiskeli na wanaotumia mbinu zingine za usafiri wanapaswa kuwa waangalifu kila wakati wanapowaribia wanaotembea kwa miguu.
- **Waendeshaji baiskeli wanapaswa kutumia upande mmoja.** Kupeana nafasi ni kuwajali wengine, na njia bora ya kuwapa nafasi wanaotembea kwa miguu ni kwa kutumia upande mmoja! Ikiwa unahitaji kumpita mtu, hakikisha kwanza ni salama kufanya hivyo. Chukulia ni kama kuendesha gari kwenye barabara ambapo magari yanapishana, unapaswa kumpita tu aliye mbele ikiwa ni salama.
- **Waendeshaji baiskeli wanapaswa kumjulisha aliye mbele wanapotaka kumpita.** Kusema “passing on your left” (“napita upande wako wa kushoto”) na kupiga kengele, ikiwa ipo, ni desturi nzuri. Hii huwawezesha watu walio

mbele yako kujua upande unaotumia kwa sababu wanaotembea kwa miguu na baiskeli nyingi hazina vioo vya kutazama nyuma.

- **Tii ishara za trafiki.** Waendeshaji baiskeli sharti watii taa za trafiki na ishara kama vile alama ya kusimama, kupeana nafasi na vivuko vya wanaotembea. Utiifu huu huwalinda watumiaji wote wa barabara na huwawezesha kuelewa wanachopaswa kufanya.
- **Wanaotembeza mbwa sharti watumie mkanda mfupi** na wahakikishe mbwa hazuii waendeshaji baiskeli na watu wengine wanaotumia Njia. **Kumbuka kuondoa kinyesi cha mbwa wako.** Kuondoa kinyesi hudumisha usafi wa Ziwa na Njia Iliyozingirwa na Miti.
- **Kuwa salama unapoendesha.** Vaa kofia na vifaa vya kujikinga unapoendesha baiskeli, skuta au viatu vya magurudumu. Washa taa unapoendesha baiskeli usiku.

Tafadhali tunza bustani zetu

- Usichume maua, matunda au matawi, wala usiharibu au kung'oa mmea au kitu chochote katika bustani za mji.
- Usitupe takataka
- Usije na chupa za glasi kwenye bustani (isipokuwa unapopiga kambi North Beach)
- Usipige kambi popote, isipokuwa North Beach Campground
- Usiwashe fataki zozote
- Usije na bunduki kwenye bustani
- Usiwashe moto (Sheria za Mji haziruhusu uwashaji moto popote kwenye mji)
- Usiruhusu mbwa kukimbia kila mahali, isipokuwa katika maeneo maalum yaliyotengewa mbwa
- Usivute sigara katika sehemu za kuchezea, kwenye makazi, ufuo, ngazi au uwanja wa riadha
- Usije na mbwa kwenye fuo za umma katika Oakledge Park, North Beach au Leddy Beach

Huenda ukahitaji idhini

Katika hali zifuatazo, unahitaji idhini maalum kutumia bustani

- Ikiwa kuna kundi la watu ishirini (20) au zaidi wanaotaka kutumia eneo au sehemu fulani ya bustani.
- Ikiwa unahitaji kuhifadhi nafasi na kutumia eneo au sehemu maalum ya bustani bila watu wengine kwa muda na tarehe mahususi au ikiwa ungependa kuratibu matumizi ya mara kwa mara.
- Iwapo ungependa kutumia eneo au sehemu fulani ya bustani kufanya hafla inayoshirikisha umma
- Iwapo ungependa kutumia eneo au sehemu fulani ya bustani kwa madhumuni ya kibiashara au kuchangisha fedha
- Mashindano ya spoti au michezo ambapo watu binafsi au timu zinatozwa ada ya kushiriki au kutazama
- Ikiwa wewe ni mtumbuizaji na ungependa kutumia sehemu fulani ya bustani kwa shughuli ambapo huenda ukachangisha pesa au ukahitaji watu walipie ada fulani

Mbwa kwenye Bustani na Ufuoni

- Unaruhusiwa kuingia na mbwa katika bustani zetu na maeneo yetu ya umma, lakini **sharti umfunge mkanda**
- Mbwa HAWARUHUSIWI kwenye fuo zetu za kuogelea za umma (Oakledge/Blanchard, Leddy, North Beach)
- Pata maelezo zaidi kuhusu maeneo unayoweza kumpeleka mbwa wako.

Sheria kuhusu Maeneo Yaliyotengewa Mbwa

Hufunguliwa Asubuhi hadi Jioni

Sheria kwa mwenye mbwa:

- Furahia wakati wako katika maeneo yaliyotengewa mbwa. Waheshimu watu wote na uwe jirani mwema.
- Unawajibikia mbwa wako
- Saidia kudumisha usafi wa eneo na uondoe kinyesi cha mbwa wako. Weka takataka kwenye mapipa na usitupe uchafu ovyo.
- Mbwa wote, na watoto chini ya miaka 12, sharti waandamane na mtu mzima wa miaka 18 au zaidi.

- Hupaswi kuleta zaidi ya mbwa watatu (3).
- Ni vyema kwa mbwa wako kuwa na leseni na kuchanjwa kulingana na sheria.
- Eneo hili ni la mazoezi ya mbwa pekee.
- Tafadhali usije na chakula cha mbwa.
- Sharti mbwa aweze kutii anachoelezwa. Tafadhali hakikisha mbwa ana mkanda kila wakati.
- Tafadhali usiruhusu mbwa kuchimba, isipokuwa katika eneo lililotengwa. Funika shimo lolote ambalo mbwa amechimba.
- Mbwa wakubwa hawaruhusiwi katika eneo la mbwa wadogo.
- Mbwa katili/wakali au mbwa wa kike wenye hamu hawaruhusiwi.
- Huruhusiwi kunywa pombe au kuvuta sigara kwenye bustani.
- Ukiumwa na mbwa YEYOTE sharti uripoti mara moja kwa Idara ya Polisi ya Burlington: (802) 658-2704. Piga 911 ikiwa kuna Dharura.

Sheria kuhusu mbwa:

- Tafadhali punguza kubweka. Mbwa haruhusiwi kuchimba. Mbwa haruhusiwi kuwadhuru mbwa wengine. Kubweka!

Eneo la kutelezea

Hufunguliwa Asubuhi hadi Jioni

SHERIA:

- Kuteleza ukitumia viatu au ubao wenye magurudumu, na kufanya michezo hatari kwenye baiskeli kunaweza kusababisha majeraha mabaya: kuvunjika mifupa, kupooza, madhara kwenye ubongo au hata kifo. Kutumia ubao/viatu vya magurudumu ni hatari.
- Saidia kuzuia mikwaruzo; Skuta na baiskeli za BMX SHARTI ziwe na raba iliyofunika sehemu wazi zenye chuma, na baiskeli sharti ziwe na sehemu ya plastiki iliyochomoza kwenye magudumu au isiwe na chochote kilichochomoza.
  Inapendekezwa uvalie helmeti, vifunika magoti, vifunika kiwiko, na glavu za kulinda mkono.
- Teleza kadri uwezavyo.
- Wazazi na walezi wanawajibikia usalama wa watoto wao na kuhakikisha kwamba watoto wao wanatii sheria za bustani.
- Magari hayaruhusiwi kuingia.

- Saidia kudumisha usafi wa maeneo ya kutelezea! Tumia mapipa na usitupe takataka.
- Waheshimu watelezaji wenzako na watu wanaotazama. Usitumie lugha ya kutisha, kuudhi au matusi.
- Matuta, reli au vifaa vingine vya kibinafsi ni marufuku.
- Usitumie eneo la kutelezea ikiwa lina unyevunyevu, barafu au limefunikwa na theluji, au ikiwa kuna vifusi, takataka au vitu vingine.
- FURAHIA! Kuwa salama.

Je, ungependa kutumia Kijindege kilicho na Kamera katika Bustani zetu? Unahitaji kujua yafuatayo:

Masharti haya yamewekwa na FAA. Hatutoi idhini za kuendesha vijindege vilivyo na kamera.

1. Sajili kijindege chako, weka nambari yake ya usajili upande wa nje (PDF), na uje na stakabathi ya usajili wake.
2. Endesha kijindege kwa madhumuni ya kujifurahisha pekee.
3. Fuata mwongozo wa usalama wa shirika la kijamii.
4. **Kijindege chako kisipite futi 400 kwenda juu ukiwa katika sehemu ya anga isiyodhibitiwa au iliyoanishwa kuwa "Class G" (Daraja la G).** Kwenye sehemu hii, FAA haidhibiti trafiki ya angani. Ili kubaini daraja la anga la mahali ulipo, angalia programu ya simu ya mkononi inayodhibiti kijindege chako (ikiwa ipo) na/au tumia programu zingine husika za simu ya mkononi. Kujua eneo lako na daraja la anga la mahali ulipo pia kutakusaidia kuepuka kuhitilafiana na ndege zingine.
5. **USIENDESHE kijindege katika sehemu ya anga inayodhibitiwa (juu na karibu na viwanja vingi vya ndege) isipokuwa:**
    1. Iwe umepokea idhini mapema kutoka LAANC (Low Altitude Authorization and Notification Capability - Kitengo Kinachosimamia Ndege Zinazopaa Chinichini), inayokuruhusu kutumia kijindege katika sehemu za anga zinazodhibitiwa. Pata maelezo zaidi kuhusu Watoa Huduma wa UAS walioidhinishwa na LAANC kwa ajili ya waendeshaji wa kujifurahisha.
    2. Unatumia kijindege katika eneo maalum lililotengewa waendeshaji wa kujifurahisha na lina makubaliano yaliyoandikwa kati yao na FAA. FAA imechapisha orodha ya maeneo yaliyoidhinishwa (MS Excel) na imezionyesha kwa kutumia nukta za buluu kwenye ramani. Kila eneo

maalum lina masharti yake ya altitudo kama ilivyoonyeshwa kwenye ramani hii.

KUMBUKA: Ikiwa shirika lako lingependa kutia saini makubaliano ili kuwa na eneo maalum la kuendeshea kijindege, tafadhali wasiliana nasi kupitia 9-AJT-UAS-Integration@faa.gov.

KUMBUKA: *Bustani zote za BPRW ziko chini ya sehemu za anga zinazodhibitiwa isipokuwa Starr Farm Park.*

6. **Hakikisha unaona kijindege chako,** au kinaonekana na mwangalizi ambaye mko pamoja na anaweza kuwasiliana nawe moja kwa moja.
7. **USITUMIE kijindege katika sehemu ya anga ambapo ni marufuku.** Masharti kuhusu anga yanapatikana kwenye ramani yetu, na masharti ya muda yanapatikana hapa. Waendeshaji vijindege wanapaswa kuzingatia masharti yote ya anga.
8. Kijindege chako kamwe hakipaswi kukaribia ndege nyingine, hasa karibu na viwanja vya ndege.
9. Kamwe kijindege chako kisipite juu ya watu, penye hafla za umma, au kwenye viwanja vilivyojaa halaiki ya watu.
10. Kamwe kijindege chako kisipite mahali palipo na hali za dharura kama vile ajali, shughuli za walinda usalama, kuzima moto au juhudi za uokoaji wakati wa kimbunga.
11. Kamwe usiendeshe kijindege ukiwa umekunywa pombe au dawa za kulevya.

Wanaoendesha vijindege hivi kwa madhumuni ya kujifurahisha wanapaswa kufahamu kuwa endapo watakiuka kimakusudi mojawapo ya masharti haya ya usalama, na/au kuendesha kijindege isivyoruhusiwa na isivyostahili, huenda wakatozwa faini kwa kosa la jinai na/au la kijamii.

Kukodisha Nafasi kwenye Bustani na Majengo

Idhini ya Kutumia Bustani

Kwa Nini Unahitaji General Park Permit (Idhini ya Kawaida ya Kutumia Bustani)?

Unahitaji idhini ikiwa unatarajia watu 20 - 99 kuhudhuria hafla isiyo ya umma katika mojawapo ya bustani nyingi za Burlington! Idhini ya kawaida ya kutumia bustani haikuruhusu kutumia utakavyo nafasi uliyopewa na haikuruhusu kutumia vipaza sauti wala kuuza chochote. Iwapo ungependa kutumia utakavyo nafasi uliyopewa, unahitaji kutumia vipaza sauti na/au una wachuuzi, AU unatarajia zaidi ya watu 99, tafadhali pata zaidi hapa chini kuhusu hafla zinazohitaji Special Use Permits (Idhini Maalum ya Kutumia Bustani).

Ikiwa ungependa kuomba idhini au una swali lolote, tafadhali piga simu kupitia nambari (802) 865-7247.

TAFADHALI KUMBUKA: Ikiwa ungependa kuhifadhi nafasi kwenye mojawapo ya majengo au bustani zetu kwa madhumuni ya hafla ya kibinafsi, huhitaji general aprk permot (idhini tofauti ya kawaida ya kutumia bustani).

Kwa nini unahitaji Special Use Permit (Idhini Maalum ya Kutumia Bustani)?

- Ikiwa ungependa kuwa na hafla ya umma.
- Ikiwa wanaohudhuria hafla ya kibinafsi ni zaidi ya watu 99.
- Iwapo unahitaji kutumia utakavyo jengo au sehemu fulani ya bustani kwa muda na tarehe mahususi (yaani, kufanya hafla kwenye Battery au City Hall Park).
- Ikiwa ungependa kutumia vipaza sauti na/au una wachuuzi.
- Ikiwa ungependa kutumia bustani mara kwa mara.
- Iwapo ungependa kutumia eneo au sehemu fulani ya bustani kwa madhumuni ya kibiashara au kuchangisha fedha
- Ikiwa wanaohudhuria wanahitaji kulipia ada ya kushiriki au kutazama.
- Ikiwa wanaohudhuria wataombwa kutoa pesa wakati wa hafla.

Maombi yote ya kupata Special Use Permits (Idhini Maalum ya Kutumia Bustani) yanahitaji kuidhinishwa na Parks, Recreation and Waterfront Commission (Tume ya Bustani, Burudani, na Kingo za Maji) angalau mwezi mmoja kabla ya tarehe husika. Tume hii hufanya mkutano Jumanne ya pili ya kila mwezi (isipokuwa mwezi Julai), na waandalizi wa hafla wanahimizwa kuhudhuria mkutano huo, japo si lazima. Ili uwasilishe ombi lako kwa Tume hii, sharti uwasiliane na Idara yetu. Tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247 ikiwa una swali lolote au ili uanze mchakato huu.

Idhini Maalum ya kutumia Bustani hutolewa kwa mujibu wa Kiambatisho D cha Code of Local Ordinances (Kanuni za Mtaa). Unaweza kusoma kanuni zote hapa kwenye sehemu ya “Kiambatisho D”:

http://www.codepublishing.com/VT/Burlington/

Kufanya Shughuli kwenye Bustani

Ikiwa ungependa kufanya mipango na/au shughuli za nje kwenye bustani ya Burlington, tafadhali jaza fomu hii kisha uitume kupitia barua pepe kwa modaniel@burlingtonvt.gov. Shughuli za nje zinazohudhuriwa na watu wasiozidi 19 hazilipishwi ada ya ziada wala hazihitaji kuratibiwa mapema. Shughuli zinazohusisha watu 20 au zaidi, zinahitaji kuzingatia mwongozo wetu wa ada za "General Park Permit" (Idhini ya Kawaida ya Kutumia Bustani) kulingana na idadi ya watu na zinahitaji kuratibiwa kupitia Idara yetu.

Ikiwa una swali lolote, tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247!

Picnic Shelters (Sehemu za Tafrija) na Kukodisha Hema

Kwenye kingo za kuvutia za Lake Champlain, kuna sehemu 3 unazoweza kukodisha; 2 zinapatikana Oakledge, 1 inapatikana North Beach (1), na ipo hema 1 ya kukodishwa huko Leddy Park. Sehemu hizi zinaweza kutumika kuandaa hafla za watu wachache kama vile sherehe ya siku ya kuzaliwa, tafrija ya wafanyakazi wa kampuni na mikutano ya familia/marafiki. Unaweza kukodisha hema na sehemu hizi kwa nusu siku au siku nzima na kuanzia katikati ya mwezi Mei hadi katikati ya Septemba.

Angalia ikiwa kuna nafasi ya kukodisha sehemu ya tafrija au hema kisha utume ombi lako mtandaoni hapa. Au unaweza kutupigia simu kwa nambari (802) 865-7247 ili uhifadhi mojawapo kati ya nafasi hizi. Tafadhali kumbuka kuwa huenda saa za kazi ni chache. Tutakupigia simu au tutakutumia barua pepe haraka iwezekanavyo.

Yanayopatikana

- Meza za kulia chakula nje
- Vyoo
- Jiko la kuchomea choma
- Ina maili 9 za kuendeshea baiskeli
- Mandhari ya maji
- Iko karibu na ufuo wa umma

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe hema au sehemu ya tafrija, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Sharti utumie kadi ya malipo kuhifadhi nafasi (Visa, MC, AmEx, Discover).
- Wanyama vipenzi wanaruhusiwa, kadri ya masharti yafuatayo: a) sharti wafungwe mkanda b) sharti waangaliwe kila wakati c) wamiliki sharti wasafishe uchafu wa wanyama wao kila mahali, na d) wanyama vipenzi HAWARUHUSIWI kufika ufuoni.
- Makaa hayatumiki; Unaruhusiwa kuleta jiko la gesi la kuchomea nyama.
- Pombe inaruhusiwa lakini chupa za glasi na mapipa hayaruhusiwi.
- Weka makaa yenye moto mahali panapostahili.

Kanuni zinazosimamia sehemu za tafrija zimebainishwa kwenye Code of Ordinances (Kanuzi za Mtaa) ya City of Burlington (Mji wa Burlington), Sheria na Masharti ya Burlington Parks, Recreation, and Waterfront Department (Idara ya Mbuga, Bustani na Kingo za Maji).

Matukio kwenye Battery Park

Battery Park Band Shell imetengwa kwa ajili ya sanaa ya uigizaji, tamasha, hotuba, maandamano, sherehe za kiraia na maonyesho, na unaweza kukodisha kuanzia mwezi Mei hadi katikati mwa Oktoba.

Yanayopatikana

- Umeme
- Vyoo
- Mandhari ya Maji

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe bustani, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Ili uruhusiwe kufanya hafla yoyote kwenye Battery Park, unahitaji Idhini Maalum ya Kutumia Bustani. Tafadhali angalia sehemu ya **Park Permits (Idhini ya Kutumia Bustani)** katika ukurasa huu ili upate maelezo zaidi.
- Ikiwa unatumia spika kwenye bustani, sauti haipaswi kuzidi desibeli 75 na unapaswa kutumia vipaza sauti kati ya 9am na 9pm. Kila siku, muda mrefu zaidi unaoruhusiwa ni saa 3. Maombi yote sharti yaidhinishwe na Parks, Recreation and Waterfront Commission (Tume ya Bustani, Burudani, na Kingo za Maji).
- Sharti umfunge mbwa mkanda kila wakati.

- Unahitaji Cheti cha Bima kwa hafla zote.
- Unahitaji kukodisha choo cha kubebeka ikiwa wanaohudhuria ni watu 50 au zaidi.
- Magari hayaruhusiwi kuingia katika bustani.

Ikiwa una swali lolote kuhusu kuhifadhi nafasi kwenye Battery Park, tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247.

Matukio kwenye City Hall Park

Baada ya miaka mingi ya ujenzi, City Hall Park imekarabatiwa na iko tayari kutumika tena na watu wote! Eneo hili lina mengi yaliyoboreshwa na linaweza kutumiwa kwa hafla ndogo na wastani, za umma na za kibinafsi.

Yanayopatikana

- Choo kimoja cha nje, cha watu wote
- Bustani ya maji ambayo hutumiwa na watu wote wakati mwingine
- Meza na viti vya nje ambavyo hutumiwa na watu wote wakati mwingine
- Umeme na intaneti (utalipia ada ya ziada)
- Viunzi/Vizuizi (utalipia ada ya ziada)
- Spika (utalipia ada ya ziada)
- Skrini za Video (utalipia ada ya ziada)

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe bustani, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Ikiwa unatumia spika kwenye bustani, sauti haipaswi kuzidi desibeli 75 na unapaswa kutumia vipaza sauti kati ya 9am na 9pm. Kila siku, muda mrefu zaidi unaoruhusiwa ni saa 3. Maombi yote sharti yaidhinishwe na Parks, Recreation and Waterfront Commission (Tume ya Bustani, Burudani, na Kingo za Maji).
- Unahitaji Cheti cha Bima kwa hafla zote.
- Huenda ukahitaji kukodisha choo cha kubebeka kwa hafla zote.
- Sharti umfunge mbwa mkanda kila wakati.

Ikiwa una swali au ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu kukodisha City Hall Park, tafadhali tuma barua pepe kwa aclawson@burlingtoncityarts.org.

Matukio kwenye Waterfront Park

Waterfront Park ni bustani kubwa ya kieneo iliyoko magharibi mwa jiji kando ya Lake Champlain Shoreline. Hafla kadhaa kubwa hufanyika kwenye bustani hii msimu wa Machipuko, Kiangazi na Mapukutiko, na Burlington Bike Path (Njia ya Baiskeli) iko kwenye mpaka wake wa kushoto. Ili upate maelezo zaidi kuhusu ada na mchakato wa kukodisha Waterfront Park kwa hafla ya umma au ya kibinafsi, tafadhali tuma barua pepe kwa rbailey@burlingtonvt.gov.

Kutembea na Kukimbia

Sasa tunapokea maombi ya mwaka wa 2022 kwa wanaotaka kushiriki katika kutembea/kukimbia. Tafadhali tuma fomu yako ya ombi (imeambatishwa hapa chini) au maswali kwa modaniel@burlingtonvt.gov. Maombi yatashughulikiwa kulingana na yanavyopokelewa. Tafadhali kumbuka kuwa, sharti ulipe ada ya kuwasilisha ombi ya dola 50 kabla ya ombi lako kukaguliwa. Ikiwa una swali lolote, tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247.

Bofya hapa ili upakue fomu ya maelezo na ombi

Burlington Greenway

Burlington Greenway (Bike Path, Njia ya Baiskeli) ina umbali wa maili 8, inapatikana kwenye kingo za Lake Champlain na ni sehemu ya Island Line Trail ambayo ina umbali wa maili 14 na inaunganisha Burlington, Colchester Causeway, na Allen Point Access Area.

Greenway inaanzia kusini kwenye Queen City Parkway na kupanda kaskazini hadi Colchester kwenye kivuko cha Winooski River. Imetengewa tu wasiosafiri kwa magari, na licha ya kutumika kwa madhumuni ya kujifurahisha, pia inatumika kwa usafiri kwani mamia ya watu hupitia njia hii kila siku. Greenway pia inaunganisha bustani, hifadhi na fukwe nyingi za umma na ni kivutio maarufu cha watalii kuanzia upande wa chini wa mji kwa mashua au feri kupitia bandari ya Burlington.

Ada

Burlington Greenway inatumika tu kwa matukio maalum yaliyoidhinishwa na Idara.

Yanayopatikana

Burlington Greenway inapitia Oakledge Park, Lakeside Park, Roundhouse Park, Perkins Pier, Waterfront Park, Waterfront Access North, Urban Reserve, North Beach, Arms Park, Leddy Park, na Starr Farm Park. Mengi yanapatikana kwenye bustani hizi.

Mara kwa mara, kuna choo kwenye Oakledge, Waterfront Park, North Beach na Leddy Park.

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe Greenway, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Magari hayaruhusiwi kwenye Greenway.
- Wanyama vipenzi wanahitaji kufungwa mkanda. Kuna sehemu mbili zilizotengewa mbwa kwenye njia hii katika Urban Reserve na Starr Farm Park.
- Wanyama vipenzi hawaruhusiwi kwenye fukwe za umma.
- Tafadhali tii alama za trafiki na vivuko vyote vya barabarani.
- Huruhusiwi kuwaomba watu bila idhini.

Sheria na masharti ya Greenway yamebainishwa kwenye Code of Ordinances of the City of Burlington (Kanuni za Mtaa za Mji wa Burlington), Sheria na Masharti ya Burlington Parks, Recreation, and Waterfront Department (Idara ya Mbuga, Bustani na Kingo za Maji za Mji wa Burlington), http://www.burlingtonvt.gov/Attorney/Municipal-Code.

Tutumie barua pepe ikiwa una swali kuhusu kuhifadhi nafasi kwenye Greenway.

Kufanya Harusi kwenye Bustani

Je, ungependa kufanya harusi katika mojawapo ya bustani zetu nzuri? Yafuatayo ni maelezo ya jumla ya kukusaidia kubaini ikiwa chaguo zinazopatikana zinakufaa:

- Kwa sherehe zinazohudhuriwa na watu wasiozidi 100 na hakuna vitu vitakavyotumiwa (yaani viti, hema, n.k.) wauzaji au vipaza sauti, utalipia ada ya Idhini ya Kawaida ya Kutumia Bustani. Tafadhali angalia sehemu ya **Park Permits** (**Idhini ya Kutumia Bustani)** hapa juu ili upate maelezo zaidi.
- Sehemu ya nje (yaani sehemu ya tafrija) sharti ikodishwe ili kuandaa hafla inayohusisha vitu mbalimbali, wauzaji au vipaza sauti na/au sherehe ya aina yoyote. Tafadhali angalia sehemu ya **Picnic Shelters** (**Sehemu za Tafrija)** hapa juu ili upate maelezo zaidi. Hii haitumiki ikiwa unakodisha Waterfront Park kwa ajili ya harusi yako.

- Huhitaji idhini ya kupiga picha au kurekodi video kwa ajili ya picha za harusi/uchumba.

Yafuatayo ni maeneo maarufu ambako unaweza kufanyia harusi:

- Battery Park
- Ethan Allen Park:
    - The Pinnacle (hakuna njia ya magari inayofika hapa - wote wanaohudhuria wanahitaji kutembea/kuendesha baiskeli kwenda huko)
- Oakledge Park:
    - Blanchard Beach
    - Oakledge Cove
    - Treehouse (huhitaji idhini kutumia eneo hili, lakini anayefika wa kwanza anapata fursa kuitumia kabla ya wengine, na lazima isalie wazi na iweze kutumiwa na watu wote kila wakati)
- Waterfront Park
- Louisa Howard Chapel

Ili upate maelezo zaidi kuhusu mchakato wa kupata idhini na kuhifadhi nafasi au ikiwa una swali kuhusu eneo na tarehe, tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247!

Viwanja vya Riadha

Unaweza kukodisha viwanja vya riadha katika bustani zifuatazo:

- Calahan Park: Uwanja wa Riadha Unaotumika kwa Michezo Mingine, Viwanja vya Besiboli/Softiboli
- Leddy Park: Uwanja wa Riadha Unaotumika kwa Michezo Mingine, Viwanja vya Softiboli ya Vijana na Watu Wazima
- Starr Farm Park: Viwanja vya Riadha Vinavyotumika kwa Michezo Mingine
- Roosevelt and Shiffilliti Park: Viwanja vya Besiboli/Softiboli ya Vijana

Kuhifadhi nafasi

Ikiwa una swali lolote au ungependa kutuma ombi, tafadhali piga simu kwa nambari (802) 865-7247. Katika kuhifadhi nafasi ya uwanja mjini Burlington, shule na shughuli zinazohusiana na bustani ndizo hupewa kipaumbele.

Yanayopatikana

- Mapipa/Kontena za Taka Inayoweza Kutumika Upya
- Vyoo

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe uwanja wa riadha, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Huenda ukahitaji nambari ya kadi ya malipo.
- Huruhusiwi kutumia uwanja wa riadha wakati wa mvua.
- Huruhusiwi kuweka kitu kinachoweza kudunga, kuchora mistari, goli, nk.
- Huruhusiwi kutumia vipaza sauti bila idhini.
- Viwanja vya riadha vinapaswa kutumiwa kwa madhumuni ya burudani pekee.
- Mechi au mchezo wowote uliopangwa na unaoshirikisha zaidi ya watu 20 unahitaji ukodishaji rasmi wa uwanja.

Kanuni za viwanja vya riadha zimebainishwa kwenye Code of Ordinances of the City of Burlington (Kanuni za Mtaa za Mji wa Burlington), Sheria na Masharti ya Burlington Parks, Recreation, and Waterfront Department (Idara ya Mbuga, Bustani na Kingo za Maji za Mji wa Burlington), http://www.burlingtonvt.gov/Attorney/Municipal-Code.

Miller Community & Recreation Center

Miller Center inapatikana karibu na Hunt Middle School na CP Smith Elementary School kaskazini mwa Burlington na ina mengi ikiwemo:

- **Ukumbi wa Mazoezi** – Uwanja wa mpira wa vikapu wa shuleya upili wenye ukubwa wa futi 7,000 mraba ulio na sakafu laini, viti vinavyohamishika vya watu 70, ubao wa kielektroniki, magoli ya mpira wa vikapu yanayoweza kundolewa, kigawanyishaji cha ukumbi wa mazoezi, na vyumba vya kubadilishia nguo vyenye vyoo, bafu na kabati.
- **Ukumbi wa Jumuiya** – nafasi ya kutosha ya ukubwa wa futi 1,800 mraba, projekta na skrini ya juu, sauti mviringo, meza na viti, ina nafasi ya hadi watu 120. Ina jikoni ndogo ya maandalizi na mapishi kwa wahudumu.
- **Chumba cha Watoto** – Kinachoweza kutumika kwa sherehe ya siku ya kuzaliwa na pia mikutano ya watu wachache. Chumba hiki kina sinki na kaunta, vifaa vya kuchezea, kabati na meza na viti vya watoto. Maktaba Yetu ya Fletcher Free Library “Micro Library” pia ipo kwenye Chumba cha Watoto – jisikie huru kuazima kitabu unapoitembelea! Ina nafasi ya hadi watu 25.

- **Studio ya Mazoezi** – Iko karibu na ukumbi wa mazoezi, ina ukubwa wa futi 1,100 mraba, sakafu ya mbao, vioo kwenye ukuta, muziki na mwangaza mwingi kutoka nje. Nafasi ya watu inategemea shughuli.
- **Chumba cha Sanaa** – Chumba hiki pia kipo karibu na ukumbi wa mazoezi na kina kaunta, sinki, meza na viti vya hadi watu 30.
- **Chumba cha Mikutano** – Kipo mkabala wa ukumbi, kina mandhari tulivu na watu wote wanaruhusiwa kukitumia BILA MALIPO kwa ajili ya mikutano, n.k, kina nafasi ya hadi watu 12, BILA MALIPO.

Unaweza kughairi nafasi uliyohifadhi wiki mbili kabla ya tarehe ya tukio. Ukighairi chini ya siku 14, utatozwa ada kamili isipokuwa chumba kikodishwe na mtumiaji mwingine. Unahitaji kulipa pesa zote za ukodishaji unapohifadhi nafasi, isipokuwa kama mkubaliane vinginevyo na mhudumu wa Miller.

Tutumie barua pepe ili uhifadhi nafasi kwenye Miller Recreation Center.

Leddy Ice Arena

Unaweza kukodisha viwanja vya barafu kwa ajili ya utelezaji. Pia tuna Ukumbi mkubwa unaoweza kutumika kwa hafla kama vile sherehe za siku ya kuzaliwa.

Tutumie barua pepe ili uhifadhi nafasi kwenye leddy Ice Arena.

The CORE (Center of Recreation & Education) at the ONE Community Center (CORE (Kituo cha Burudani) na Elimu kwenye ONE Community Center)

IBPRW inasimamia ghorofa ya pili ya ONE Community Center kwenye 20 Allen Street eneo la Old North End. Tuna madarasa kadhaa, kumbi za jumuiya na ukumbi wa mazoezi unaokodishwa. Ikiwa ungependa kupata maelezo zaidi, tafadhali piga simu kwa nambari 802-865-7088.

Schmanska Barn

Inapatikana Mashariki mwa Burlington kwenye Schmanska Park na ni ya kukodishwa! Inaweza tumika kwa sherehe za kibinafsi za watu wachache, mikutano ya jumuiya au mikutano ya kibiashara. Schmanska Barn inakodishwa mwaka mzima, na ina nafasi ya

watu 60 katika msimu wa Mchipuko, Kiangazi na Mapukutiko, na watu 30 katika msimu wa Baridi. Unapokodisha mahali hapa, unahitajika kufungua, kusafisha na kufunga baada ya kutumia. Utapewa idhini ya kutumia Nyumba pamoja na maagizo ya mwanzo ndani ya saa 48 baada ya kukodisha, na pia kuna fomu ya “Maagizo ya Kukamilisha” unayopaswa kujaza mtandaoni muda wako unapokwisha. Kila Nyumba inapotumika, itakaguliwa ili kuona usafi wake na hali yake.

Ikiwa una swali au ungependa kutuma ombi, tafadhali tutumie baua pepe kwa modaniel@burlingtonvt.gov

Yanayopatikana

- Choo
- Umeme
- Meza 10 (za ukubwa tofauti)
- Viti 30 Vinavyokunjika
- Kipasha Joto katika Msimu wa Baridi
- Vifaa vya Kusafisha
- Mandhari ya nyasi mbele ya Barn

Sheria na Masharti

- Ili ukodishe nyumba, sharti uwe umefikisha miaka 18.
- Lazima uzingatie utaratibu za kufungua na kufunga/kusafisha.
- Sharti ulipie nafasi wakati wa kuweka nafasi.
- Anayekodisha atawajibika uharibifu wowote utakaotokea wakati wa kuhifadhi nafasi.